

Nambari ya Mtahiniwa _____

CKAICS

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU

202

KISWAHILI

MUDA: SAA 2:30

JUMATANO 23 OKTOBA 2024 MCHANA

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C, na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



2092427

Mtihani huu una kurasa 15 zenye maandishi

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Nimechoka sumbuliwa,
Nami kazi naijua,
Shoka na mundu tanoa,
Natia jembe mpini,

kwa mihogo vikapuni,
liniwekalo ni nini,
nijitose aridhini,
nirudie kazi yangu.

Chakula cha kununua,
Mchele wa kupimiwa,
Nimechoka kukemewa,
Natia jembe mpini,

hakina tamu kinywani,
kilo moja kwa thumuni,
na matajiri dukani,
nirudie kazi yangu.

Asubuhi ikifika,
Nabaki kuhangaika,
Nawambia kwa hakika,
Natia jembe mpini,

hamna kitu tumboni,
cha kukila sikioni,
uvivu ni kitu duni,
nirudie kazi yangu.

Mshahara nikipata,
Kwa mengi mno matata,
Njiani siwezi pita,
Natia jembe mpini,

haungii mfukoni,
yaliyo daftarini,
madeni hadi kooni,
nirudie kazi yangu.

Jamani nataka lima,
Kunde choroko mtama,
Jua likeshanichoma,
Natia jembe mpini,

mihogo ya matutani,
na mpunga mabondeni,
panga taweka kwapani,
nirudie kazi yangu.

Wala sishiki la mtu,
Wanaadamu si kitu,
Kilimo ni kazi yetu,
Natia jembe mpini,

hayangii akilini,
wakutosa baharini,
tangu kale za manani,
nirudie kazi yangu.

MASWALI

a) Mwandishi wa shairi hili alianza kufanya kazi gani?

b) Taja sababu iliyopelekea mshairi kutoa uamuzi wa kurudia kazi yake ya zamani.

c) Andika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyopigiwa mstari.

- i. _____
- ii. _____

d) Taja mazao mawili (2) ambayo mshairi anakusudia kuyalima.

- i. _____
- ii. _____

e) Toa ujumbe mmoja (1) unaopatikana katika shairi ulilolisoma hapo juu.

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno yasiyozidi ishirini (20).

Watoto wengi sana huweza kusoma vyema mara wanapoanza Skuli. Madrasa ni sehemu nyengine ambayo humsaidia mtoto kuweza kusoma. Kuna ulazima wa kuwafundisha watoto wetu kusoma hata wakiwa nyumbani. Wazazi wanatakiwa kuchukua hatua za makusudi katika kuwasaidia watoto wao kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu kabla hawajaandikishwa kwenye mfumo rasmi wa elimu. Mazingira ya nyumbani yana nafasi kubwa ya kumuwezesha mtoto kujifunza kusoma.

SEHEMU B: (Alama 30)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.

3. a) Bainisha viambishi awali, mzizi na viambishi tamati katika maneno yafuatayo. Mfano: anakwenda

a, na - viambishi awali

kwend - mzizi

a - Kiambishi tamati

- i. Wanapatikana

- ii. Mchezo

- b) Bainisha mofimu yenye kutambulisha nafsi ya kwanza katika maneno yafuatayo.

- i. Tunamsaidia

Nambari ya Mtahiniwa _____

ii. Nimejifundisha

c) Tunga sentensi kwa kutumia vielezi vifuatavyo.

i. polepole

ii. lini?

d) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Mwanafunzi hodari amepewa zawadi.

ii. Yule anapenda kusoma.

iii. Saade ndiye mwalimu wetu.

e) Unda neno moja kwa kila neno ulilopewa kwa kutumia mnyumbuliko.

i. Soma

ii. Salamu

4. a) Badili nomino zifuatazo kuwa vitenzi.

i. Wimbo _____

ii. Mlo _____

iii. Ndoto _____

b) Kwa kutumia mifano taja aina mbili (2) za vivumishi.

i. _____

ii. _____

c) Eleza maana ya istilahi zifuatazo.

i. Mofimu

ii. Misimu

d) Ainisha njeo zilizopigiwa mstari katika maneno yafuatayo.

i. Atakwenda

ii. Anajitayarisha

iii. Wameshamchukua

e) Tafautisha kwa kutumia mifano kati ya vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi.

5. a) Toa maana mbili (2) zinazopatikana katika neno “mbuzi”.

- b) Bainisha mazingira na watumiaji wa rejesta zifuatazo.

- i. Kula kichwa hicho, gepu hilo, usiniletee makumbi.

- ii. Unahukumiwa, umekutwa na hatia, mshtakiwa, ndugu wakili, kula kiapo.

- c) Toa maana za misimu ifuatayo.

- i. Bodaboda

- ii. Ubuyu

- d) Eleza sifa mbili (2) za lugha ya mazungumzo.

- i. _____

- ii. _____

e) Taja aina mbili (2) za watumiaji wa kamusi.

i. _____

ii. _____

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.

6. a) Nini maana ya mashairi ya kimapokeo?

b) Tunga beti mbili (2) za shairi la kimapokeo kuhusu "Umuhimu wa elimu"

7. a) Toa tafauti ya methali na vitendawili.

b) Bainisha njia tatu (3) za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

i. _____

ii. _____

iii. _____

c) Taja vigezo viwili (2) vya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi.

i. _____

ii. _____

d) Eleza kwa ufupi maana ya istilahi zifuatazo.

i. Muundo

ii. Mtindo

e) Fafanua vipera viwili (2) vya hadithi.

8. a) Mashairi, tenzi, nyimbo na ngonjera ni vipera vya utanzu gani wa Fasihi simulizi?

- b) Toa maana ya nahau zifuatazo.

- i. Amepata jiko

- ii. Amevaa miwani

- c) Fafanua vipengele vifuatavyo vya ushairi.

- i. Kibwagizo

- ii. Vina

- d) Eleza kwa ufupi maana ya methali zifuatazo.

- i. Kidole kimoja hakivunji chawa

- ii. Haba na haba hujaza kibaba
- _____
- _____
- _____
- _____
- e) Bainisha tafauti mbili (2) zinazojitokeza kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.
- _____
- _____
- _____
- _____
- _____
- _____
- _____

SEHEMU D: (Alama 20)

UANDISHI

Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii.

9. Andika insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150 juu ya mada moja kati ya zifuatazo.

- i. UMUHIMU WA KUTUNZA MAZINGIRA
- ii. MADHARA YA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

This image shows a full page of blank, lined paper. It features approximately 20 evenly spaced horizontal grey lines across the entire width of the page, providing a guide for handwriting or typing. The background is a solid off-white color.

[illegible]

10. Kwa kutumia mifano, fafania muundo wa barua ya kirafiki.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

